## Utangulizi

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, lengo kuu likiwa ni kulida Afya ya Jamii kwa kuzuia madhara yanayoweza kusababishwa na matumizi ya bidhaa hizo.

Moja ya majukumu ya TMDA katika udhibiti wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi ni kutoa vibali vya kuingiza nchini na kutoa nje ya nchi bidhaa husika. Mwingizaji, awe mfanya biashara au mtumiaji binafsi anatakiwa kuomba kibali cha Mamlaka kabla ya kuingiza mzigo au bidhaa.



## Mfumo wa kuomba vibali kwa njia ya mtandao (online application system):

Mfumo wa kuomba vibali kwa njia ya mtandao (online application system) umeanzishwa kwa lengo la kusogeza huduma karibu zaidi kwa mteja na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za kiudhibiti.

## Aina za vibali vinavyoombwa kwa njia ya mtandao:

i) Vibali vya kuingiza bidhaa nchini (Import Permits).

ii) Vibali vya kutoa bidhaa nje ya nchi (Export Permits)



## Mambo muhimu ya kuzingatiwa wakati wa kutumia mfumo huu:

i) Namba ya utambulisho kutoka TMDA

ii) Nywila (password) kutoka TMDA

III) Anuani ya barua pepe inayofanya kazi (valid email address).

iv) kompyuta / Simu yenye uwezo mkubwa

v) Mtandao wenye kasi nzuri

vi) Nakala ya kielektroniki ya taarifa ya mzigo mfano ( Ankara kifani, vibali kutoka taasisi nyingine husika nk.)



## Hatua za kufuata

i) Jaza kikamilifu fomu ya usajili ya mteja (customer registration form) na kuiwasilisha ofisi za TMDA Makao Makuu, Ofisi Ndogo DSM au katika ofisi za TMDA za Kanda au kutuma kwa anwani ya barua pepe ya TMDA ili kupata namba ya utambulisho na nywila (password).

ii) Fuata maelekezo ya namna ya kuomba kibali kama ilivyoianishwa mwongozo wa mtumiaji kitabu utakachotumiwa (user manual). Mwongozo huu unapatikana pia katika tovuti ya TMDA (www.tmda.go.tz).

iii) Kabla ya kulipia ada ya kibali husika, hakikisha hatua iliyofikiwa katika ushughulikiaji wa ombi la kibali chako.

iv) Wasilisha hati ya malipo yaliyofanyika benki katika ofisi ya TMDA ambako ombi lako linashughulikiwa.

v) Chukua kibali kutoka katika ofisi ya TMDA ambako uliwasilisha ombi lako.



**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo:**


**Mkurugenzi Mkuu,**
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),
S.L.P 1253 Dodoma au 77150 Dar es salaam.
Simu+255 22 2450512/2450751/2452108
Barua pepe: info@tmda.go.tz
Tovuti: www.tmda.go.tz
**Simu bila malipo: 0800110084**
**@tmdatanzania**


**Unaweza pia kuwasiliana nasi kupitia katika Ofisi zetu za Kanda.**


**Kanda ya Ziwa**
Barabara ya Nyasaka,
Nyakato Buzuruga,
S.L.P 543,
Ilemela - Mwanza
Simu +255 28 2981224/5
Barua pepe: info.mwanza@tmda.go.tz

**Kanda ya Kaskazini**
Eneo la Sakina.
S.L.P 16609, Arusha
Simu +255 272970333/737782442
Barua pepe: info.arusha@tmda.go.tz

**Kanda ya Mashariki**
Jengo la GEPF,
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P 31356,
Dar es salaam,
Simu +255 739 226328/788470312
Barua pepe: info.easternzone@tmda.go.tz

**Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
Jengo NHIF ghorofa ya 3.
S.L.P 6171, Mbeya
Simu +255 252504425
Barua pepe: info.mbeya@tmda.go.tz

**Kanda ya Kati**
S.L.P 1253 Dodoma.
Simu +255 26 2320156
Barua pepe: info.dodoma@tmda.go.tz

**Kanda ya Kusini**
Jengo la PSSSF,
S.L.P 1447, Mtwara.
Simu: +255 232334655
Barua pepe: info.mtwara@tmda.go.tz

**Kanda ya Magharibi**
Jengo la TUWASA,
S.L.P 520, Tabora
Simu +255 262606082
Barua pepe: info.tabora@tmda.go.tz


**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority



# UTARATIBU WA KUINGIZA NA KUTOA BIDHAA NCHINI

*TMDA - Hulinda Afya ya Jamii*